Swahili

# Ushuhuda wa Bomu la Nyuklia katika Hiroshima.

Mji wa Hiroshima umekuwa na nyakati tatu za maisha: kwanza ulikuwa kitovu cha makao ya jeshi, halafu ukawa mji ulioathirika na mlipuko wa bomu na sasa ni mji wa amani. Zaidi ya miaka sitini iliyopita................ Kiasi cha zaidi ya asilimia arobaini ya mji ulikuwa na nyenzo za kijeshi. Kutoka bandari ya Hiroshima iliyo kusini mwa mji, askari wengi na vifaa vya kivita vilipelekwa kwenye vita ya "Sino-Japanese" [1930]. Mafanikio ya Japani kijeshi katika Uchina na kuikalia nchi hiyo kulisababisha mlipuko mkubwa wa................................. Hatahivyo haraka wimbi la vita liligeuka kwa upinzani dhidi ya Japani na kusababisha vita ienee katika eneo la Pasifiki. Sehemu ya mabadiliko ilikuwa ni mapambano ya "njia ya kati". Tokea hapa mpambano ulikuwa mrefu na wenye kasi ileile mpaka kufanya majeshi ya kijapani yakimbie huku yakiandamwa na kutafutwa, na mwisho ilikuwa vita ndefu, yenye madhara na kuletea majeshi yajitoe katika mpambano wa kutetea kisiwa cha Okinawa ambacho ni sehemu ya Japani. Zaidi ya hapo toka mwaka 1942 mpaka 1945 sehemu kubwa ya miji ya Japani iliharibiwa kabisa kutokana na mashambulizi ya mabomu yaliyokuwa yenye kasi ileile. Hatahivyo katika kipindi cha mda huo nimestaajabu kwanini mji wa Hiroshima ulisalimika na mashambulizi hayo na kulikuwa hakuna mashambulizi yaliyotokea angani.

Lakini mabadiliko yalitokea alfajiri ya tarehe 6 Agosti 1945 ambapo ndege moja ya kudondosha mabomu aina ya B-29 yeney jina la "Enola Gay", ilidondosha bomu moja katika mji wa Hiroshima. Ilikuwa ni bomu la Nyukilia. Baada ya hapo nimetambua kwanini mwanzo mji wa Hiroshima uliachwa kushambuliwa na mabomu. Kwa maana madhumuni ilikuwa ni kushambuliwa na bomu la Nyukilia. Zaidi ya watu 200,000 waliuawa na kiasi cha watu 300,000 walijeruhiwa au kupata ulemavu na pia kuathiriwa na mionzi hatari inayosababisha kifo. Baadaye nilipata habari kwamba jotoridi katika sehemu ambapo bomu lilitua (ground zero) lilikuwa na nyuzi za sentigredi kati ya 3,000 mpaka 4,000. Katika ulinganishi tunahitaji nyuzi za sentigredi 1,500 tu ili kuyeyusha chuma na hapa tunaweza kuona kiasi gani bomu hili lilivyokuwa na madhara makubwa. Nguvu ya upepo wa mlipuko ulikuwa na kasi ya mita 300 kwa sekunde. Binadamu hawezi akastahimili nguvu ya upepo wa kimbunga wenye kasi ya mita 50 kwa sekunde. Katika eneo lisilozidi nusu kipenyo cha kilomita 3 kutoka sehemu ya mlipuko majengo yote yaliangamizwa na kuharibiwa kabisa.

Katika wakati wa shambulio la bomu nilikuwa mwanafunzi wa miaka kumi na nne katika sekondari ya juu. Sehemu kubwa ya wanaume walikuwa wameenda kwenye vita, kwahiyo tulilazimika kufanya kazi ya ziada katika viwanda vya.................; badala ya kusoma kila siku. Nyumba niliyokuwepo siku ya tarehe 6 Agosti ilikuwa kilomita 1.7 kutoka sehemu bomu lilipoanguka ambapo niliona mwanga uliomulika ghafla. [kwa lugha ya kijapani PIKKA] kwa muda wa sekunde 0.3 (kama ulivyotolewa na wanasayansi baadaye) na baadaye nilisikia........................[kwa lugha ya kijapani ni PON]. Maramoja bomu la Nyukilia likafahamika kama bomu la PIKKA DON. Kiasi cha joto la mwanga katika muda mfupi wa mwanzo lilimuunguza mtu yeyote aliyekuwa nje ya nyumba anayoishi. Kilichofuata baada ya mwanga

kulikuwa na sauti kubwa iliyotikisa kama tetemeko kubwa la ardhi. Kwanza nilirushwa juu na mara moja ni karudi kwenye sakafu. Kwenye sakafu moshi na uchafu wa vumbi ulikuwa unakereketa kwenye pua na kufanya nipumue kwa shida. Muda si mrefu dari lilianguka na nguzo zote za nyumba zilianguka karibu nami. Kupumua kulikuwa kwa shida na nilifikiri,"Aah...nitakufa bila shaka!" Hatahivyo kwasababu nyumba yangu ilikuwa ni ya ghorofa moja tu, niliweza kuchomoka kwenda nje lakini kwa kutumia juhudi kubwa tu, (Nukuu: watu waliokuwa kwenye nyumba zenye ghorofa nyingi walikandamizwa na kuunguzwa mpaka kifo wakati sehemu za juu za ghorofa zilipoanguka). Nguo zangu zilikuwa zimeharibiwa vibaya na mwili ulijaa damu kutokana na vipande vya chupa vilivyochoma kwenye mwili wangu. Nilipoangaza sehemu mbalimbali niliona kila nyumba imeangamizwa na nilisikia watu wengi wakilia kwa sauti, "Nisaidie!" Mtu yeyote aliyesoma jarida la vikatuni (manga) lenye kichwa cha habari, "Kiganja cha mguu kiitwacho Gen" (Hadashi no Gen) anaweza kupata picha ya janga nililoshuudia. Watu wengi walikuwa wamekandamizwa na vifusi vya nyumba zilizobomoka, wakilia wakiomba msaada, lakini walishindwa kuchomoka na mwisho waliungua mpaka kufa katika mioto. Kwasababu wale waliokuwa wazima walikuwa wameumia vibaya, hakuna mtu aliyeweza kumsaidia mwenzake. Alichoweza kufanya kila mtu ni kukimbia mbali na eneo la hatari. Nilikimbia mimi na mama yangu kwenda sehemu ya karibu ya wazi ya mapumziko, kila wakati nikiangalia watu wote waliokuwa wakikimbia hatari. Nguo zao zote zikiwa zimechanika na nywele zao zilikuwa zimeviringwa na kulalia nyuma. Miaka baadaye serikali ya mji wa Hiroshima iliwaomba walionusurika na madhara ya bomu wachore picha zikionyesha hali ya kutisha iliyowakuta na picha zilikusanywa. Niliguswa na kutishwa na picha hizi zikionyesha watu walioungua na kuvimba mikono na wenye nyuso kama sanamu za kutisha. Wengine katika picha walionekana wakiwa wameshikilia utumbo uliojitokeza nje, wakijaribu kuzuia usidondoke. Baadhi walikuwa na macho yakining'inia kutoka sehemu zake. Mama mmoja alikuwa amebeba mtoto huku sikio moja likiwa halipo, huku akilia,"maskini mtoto huyu!" Ngozi za watu wengi zilizoungua ziliumuka na kupasuka huku zikining'inia kama matambala, kwahiyo hawakuweza kukunja mikono na ilibidi watembee kama punguwani huku mikono ikiwa imenyooka. Watu wengine walipoteza uwezo wa kufikiri na walibaki wakishangaa huku wakijaribu kukimbia hatari. Kuwasimamisha ilikuwa ni kuongeza uwoga wa hatari, kwahiyo kila mtu alitembea bila lengo kwa juhudi kwenda mbali iwezekanavyo.

Mwisho mioto ya mwanzo ilisambaa kwa haraka katika kona za mji ikiongeza uharibifu zaidi. Kulikuwa hakuna mtu wa kupambana na mioto kwa vile kila mtu, hasa wazima moto, walikuwa wamefariki au kuumia vibaya. Kwahiyo mji wa Hiroshima ulikuwa kama bahari ya moto na baada ya usiku kuingia ilionekana kama mbuga inayoungua. Kilichofuata kikubwa kilikuwa ni matone mazito na meusi ya mvua ya mafuta yalianguka katika mji. Yalikuwa ni meusi kwelikweli!". Baadaye wanasayansi walieleza kwamba kwenda juu angani kwa vumbi na vipande vya kifusi, katika umbali mrefu, kuchanganya na unyevu katika anga kulitengeneza mvua nyeusi na ya mafuta ambayo siyo ya kawaida. Lakini tulikuwa na furaha kunyeshewa na mvua hiii. Hatahivyo tulikuwa na ufahamu mdogo kuhusu kiasi cha mionzi iliyo katika matone ya mvua. Kudondoka

kwa matone kwenye ngozi (na mionzi!) ilifanya tuanze kusikia baridi na kutetemeka kama vile tumepata homa japokuwa ilikuwa majira ya joto. Usiku huo wengi walilala katika sehemu za wazi lakini cha kusikitisha wengi waliokuwa na majeraha walimaliza maombolezo yao na kufariki kabla ya mwisho wa siku.

Asubuhi iliyofuata nilizunguka sehemu mbalimbali za mji na mama yangu nikimtafuta baba yangu. Baadaye zaidi tukajafahamu baba yangu alikuwa akifanya kazi ya lazima karibu na sehemu bomu lilipoanguka na alifariki mara moja lakini tulipotafuta zaidi hatukuweza kutambua habari zake. Kwahiyo tuliuliza wapita njia kama walimwona. Wakati tukimtafuta nilikuwa naburuza mguu wangu. Sasa nikatambua kulikuwa kuna kipande cha pembe tatu cha chupa katika paja langu. Watu wengi waliokuwa taabani, walipotuona na kutusikia waliomba msaada kwa kusema,"Maji! Nipatie maji, tafadhali!" Muda si mrefu wengi walifariki, sio kwa kulia katika maumivu, bali kwa kukosa maji. Katika ....................naamini kwamba kiu yao ilikuwa si kiu ya kukosa maji tu, bali pia ni kiu ya ndani ya roho-kiu ambayo Kristu aliipata akiwa msalabani ambapo alilia akisema,"Nasikia kiu!" Hili kweli linawaunganisha na jinsi Kristu alivyoteseka msalabani.

Katika wakati huo tulikuwa na wazo la kuchoma miili ya watu waliofariki. Kwahiyo tulikusanya matawi ya miti mikavu na kuyaweka juu ya miili ya watu iliyokusanywa na kutia mafuta ya tatu au petroli............................mwili wa mtoto mdogo mzuri ambaye alikuwa akiishi nyumba inayofuata toka sehemu nilipokuwa naishi, pamoja na miili mingine ya watu ambao sikuwafahamu iliwekwa hapo na kuchomwa moto. Muda si mrefu hakuna kilichobaki zaidi ya mifupa. Tukio hili lilifanyika katika sehemu mbalimbali za mji. Hata mpaka leo mji wa Hiroshima unatambulika kama sehemu kubwa ya makaburi. Kwanini watu wengi walifariki wakati wa shambulizi la bomu la Nyukilia? Kabla ya shambulizi la bomu la Nyukilia karibu vijana wengi walikuwa na shughuli nyingi katika kujiweka tayari kwa mashambulizi ya mabomu ya moto kwa kubomoa majengo yanayokamata na kuungua moto kwa haraka ili kujenga kinga ya moto kuenea na kutengeneza njia za kuchomoka hatari. Hatahivyo wafanyakazi hawa walikutwa katika uwazi na kukosekana kwa majengo kulisababisha kutokuwepo kwa kinga ya madhara ya bomu la nyukilia. Mapema katika maeneo haya wazi ambapo nyumba zilikuwepo, jeshi la Japani lilipanda viazi vitamu. Kwa kustaajabu mimea hii ya viazi ilisalimika na shambulizi la bomu la Nyukilia na si muda mrefu watu walianza kula.....................yaliyopatikana juu ya ardhi.

Wiki kadhaa baadaye watu ambao walikuwa hawajapata majeraha yoyote kwenye miili na ambao walionekana wenye afya ghafla walianza kutoka damu kwenye pua na waliharisha kwa kiasi kikubwa na nywele zao zilianza kunyonyoka. Madhara haya yalisababishwa na ugonjwa wa mionzi. Bomu la Nyukilia halikuharibu majengo tu bali lilisambaza mionzi katika kona zote za mji. Mtoto wa rafiki yangu baadaye alionyesha dalili za ugonjwa unaotokana na mionzi. Mtoto huyu hakuweza kulala usiku na kwahiyo ilibidi mama yake awe macho usiku mzima. Mama kutokana na uchovu bila kukusudia alimkaripia mwanaye alale ili naye apate kupumzika kidogo. Mwanae alilia na kupiga kelele,"Mimi sikuomba ugonjwa! Sio kosa langu! Naomba unirudishie afya yangu.

Nataka kuishi zaidi. Cha kusikitisha mtoto huyu alifariki akiwa na umri wa miaka sita. Katika nyakati hizo kulikuwa na wasichana ambao tuliwaita"Mabikira wa bomu la Nyukilia" kwasababu walikuwa wameathirika kwa kuungua vibaya kwenye nyuso zao na waliishi maisha ya majonzi na upweke. Mmoja wao aliandika utenzi wenye kichwa cha habari, "Nirudishie tabasamu langu-Hohoeni yo, kaere." Utenzi huu unasomeka kama ifuatavyo: Hatima ya ukatili ninabeba kwenye mgongo wangu, Maisha ya upweke naishi, Tabasamu hili la ubikira limefifia. Kweli nakumbuka tabasamu langu, lini litarudi?

Siku hizi wanawake hawa wanaongea kuhusu hali waliopita na wanaomba amani kwa ajili ya kuyashinda majonzi yao.

Nilibatizwa kuwa Mkatoliki miaka minne baada ya shambulizi la bomu la Nyukilia na katika sala za kuombea waliofariki na katika kuomba amani, mimi binafsi nimeweza kuongozwa katika kuwa na hali ya amani ndani ya roho yangu. Kwa niaba ya wale waliopoteza maisha katika shambulizi la bomu la Nyukilia napenda kutoa ombi duniani kote, "Hakuna tena vita ya Nyukilia!"

Leo, ukiongelea kuhusu nguvu ya maangamizi, duniani kuna zaidi ya silaha milioni moja za Nyukilia mfano wa bomu lililodondoshwa katika mji wa Hiroshima. Kama msalimika na shuhuda wa bomu la Nyukilia, nauliza kwa hasira tukio lililotokea Hiroshima katika siku ya tarehe 6 Agosti 1945 na kwanini bado hatujajifunza. Kama silaha za Nyukilia zitatumika kwa kiasi kikubwa sehemu mbalimbali duniani basi jamii ya binadamu itaangamia kabisa. Vita inaharibu kila kitu lakini amani pekee inaweza kujenga tena na kurudisha kile ambacho kimeharibiwa. Tukiongelea kuhusu urafiki wa kila siku, tunatambua chuki na migongano inavunja uaminifu lakini kupitia sala na ushirikiano wa pande zote na kuelewa mapungufu yetu, tunaweza kufanikiwa kuleta amani. Natumaini juhudi kama hizo zitusukume kufikiri kuhusu nini tufanye kwa ajili ya amani duniani. Juu ya yote lazima tuendelee kusali kwa ajili ya kupata amani.

Mwisho nitapenda kumalizia mazungumzo yangu kwa nyimbo hii: Nchi yetu iliunguzwa kabisa. Katika ardhi tulizika mifupa ya familia yangu. Sasa maua meupe yanastawi hapo. Kweli, hatutasamehe mabomu mawili ya Nyukilia. Kwahiyo lazima tuzuie bomu la tatu. Katika sehemu ya nchi yetu... na sehemu zote za dunia.

IMETAFSIRIWA NA :EPHREM MBOGOMA